**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**

Shule ya Sekondari Mailisita,
S.L.P 1734
**MOSHI**

Tarehe...................

**Kumb.Na.MSSS/JI/FI/12**
JINA LA MWANAFUNZI....................................................
S.L.P..........................................................................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAILISITA KATIKA WILAYA YA HAI, MKOA WA KILIMANJARO (JOINING INSTRUCTIONS) KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

## 1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukuarifu kwa kuchaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza mwaka **2021** hapa Shule ya Sekondari Mailisita.Shule ya sekondari Mailisita ipo katika wilaya ya Hai,Tarafa ya Lyamungo,Kata ya Mnadani,Kijiji cha Shirinjoro.Ni umbali wa mita mia tatu kutoka barabara kuu ya Moshi-Arusha. Shule ipo upande wa mashariki kutoka mji mkuu wa Moshi karibu na Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Hai.

Masomo unayotarajia kujifunza hapa shuleni ni Uraia,Kiswahili,Kiingereza,Hisabati,Historia,Jiografia,Biolojia,Fizikia,Kemia na masomo mengine ambayo utaelekezwa hapa shuleni.

Muhula wa kwnza unaanza tarehe. **11/01/2021** na unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **05/01/2021** Saa 1:15 Asubuhi na mwisho wa kuripoti ni tarehe **11/01/2021**. ndani ya siku 7

## 2.1 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

I. **SARE YA SHULE:**

a) **Sare ya Shule hii ni:-MVULANA**: Suruali 2,Shati 2,sweta 1,T-shirt 1,Soksi fupi nyeupe jozi 2 au zaidi (zisiwe na mapambo) ,viatua vya ngozi vyeusi vyenye visigino vifupi na view vya kufunga kamba(visivyo vya mapambo)

**MSICHANA**: Sketi 2, shati 2, sweta 1, T-shirt 1, Soksi fupi nyeupe jozi 2(zisiwe na mapambo),viatu vyeusi vyenye visigino vifupi na viwe vya kufunga kamba(visivyo na mapambo). Rangi ya kitambaa cha suruali na sketi ni **Damu ya Mzee** (Imeambatanishwa kwenye fomu hii),rangi ya shati ni nyeupe kama kawaida. Mzazi unasisitizwa umshonee mwanao sare .

Kwa kuzingatia maelekezo ya mashono .Aidha utaelekezwa mshono siku ya kuchukua fomu hii.Endapo utashona sare tofauti na maelekezo ,mwanao hatapokelewa.

NB: Sketi ya rinda box yenye beli ndogo ndefu(chini ya goti).

Suruali pana ya kufunga kiunoni na mkanda mweusi.

b) Rangi ya Tisheti ni njano yenye kola ya mistari meusi(Form Six)
c) Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule(nyeupe) ifunike Kiwiko cha mkono
d) Sare ya michezo ni jezi ya bluu(tisheti na kaptula kwa wavulana jozi 1) na bukta na tisheti ya rangi ya zambarau(purple) kwa wasichana jozi 1.

**2.2 VIFAA VYA DARASANI**

1. Madaftari makubwa 10 na madogo 9(kwaajili ya Test)
2. Kibeta(Mathematical set) 1
3. Chenezo(Ruler) 1
4. Kalamu ya wino na risasi

**2.3 VIFAA VYA CHAKULA**: Sahani,Kijiko na Bakuli vya bati(stainless steel)

**2.4.** Chakula cha wanafunzi,nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu

**2.5. VIFAA VYA USAFI**

1. Ufagio wa chelewa 1
2. Ndoo ndogo ya Lita 10
3. Brush 1
4. Jembe na Mpini wake
5. Fyekeo

**3.0. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Shule Inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia namba 10 ya mwaka 1995. Aidha,Inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia,yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu.

**3.1.** Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni/katika fomu hii.

**A. HESHIMA**

I. Wanafunzi wote hawana budi kuonyesha heshima mahali popote wanapokuwa shuleni na nje ya shule.
II. Ni lazima wanafunzi kuheshimu na kutii viranja na viongozi wengine.
III. Ni lazima wanafunzi kupendana na kuheshimiana wao kwa wao
IV. Ni lazima wanafunzi waheshimu na kutii walezi wake,walimu wote na wafanyakazi wasiokuwa walimu.
V. Ni lazima wawaheshimu wageni wote wanaokuja shuleni na kuwasaidia inapolazimu.
VI. Ni muhimu mwanafunzi kutii kengele na mahali anapotakiwa.
VII. Mwanafunzi atunze mali za shule/umma kwa umakini mkubwa na wenzie. Wizi ,uzembe na udanganyifu ni makosa makubwa.

VIII. Kila mwanafunzi afahamu ameingia hapa kujifunza na kujilea katika utu bora,ili mwanafunzi ajiheshimu,ajifunze na kufanya kazi kwa bidii.

**B. MAHUDHURIO**

I. Mwanafunzi anatakiwa kuwepo shuleni kwa muda wote wa saa za shule (1:15 Aaubuhi hadi saa10:30 Jioni)

II. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi na kushiriki katika shughuli zote za shule kama usafi na mazingira ,shughuli zote za uzalishaji mali,michezo n.k atakayechelewa au kukosa ataadhibiwa

III. Mwanafunzi anatakiwa kuitika mara moja na kukimbia mahali atakiwapo asikiapo kengele au mwito mwingine wowote

IV. Ni lazima mwanafunzi awahi shuleni katika tarehe alizopangwa mwanzoni mwa kila muhula au baada ya mapumziko ya aina yoyote.

**NB**:Ruhusa ya kutokuwepo shuleni siku moja au zaidi ni lazima itoke kwa Mkuu wa Shule au Makamu wake. Mzazi/Mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye atayehusika kumwombea mwanafunzi ruhusa na siyo mtu mwingine.

**C. USAFI BINAFSI**

**I. Ni lazima mwanafunzi kutunza usafi wa mwili ,mavazi na usafi wa mazingira ya shule .**

**II. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa shuleni.**

**D. MIPAKA YA SHULE**

Mipaka ya shule ni eneo lote la shule kama itakavyotambulishwa na shule. Wanafunzi wanatakiwa kuwepo ndani ya mipaka ya shule muda wote wa masomo na kufuata njia sahihi ya kupita awapo shule na baada ya masomo.Ruhusa kutoka nje ya shule wakati wa masomo itatolewa na mwalimu wa zamu,Mwalimu wa darasa au viongozi wa shule.

**E. UTARATIBU WA MASOMO**

I. Siku za masomo ni kila siku ya Jumatatu hadi Ijumaa. Mwanafunzi anatakiwa awahi shuleni kila siku asubuhi saa 1:15 ''rollcall", usafi na matangazo muhimu

**II.** Anatakiwa kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

**3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHWA KUFUKUZWA /KUSIMAMIHWA SHULE**

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile:-Bangi,Coceini,Mirungi,Kuberi n.k
e) Kupigana/kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

g) Kudharau bendera ya Taifa
h) Kuwa na ujauzito/kupata mimba
i) Kuoa/kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma,Kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi

**4.2 MAMBO MENGINE YA MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

a) Maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mzazi/mlezi wa mwanafunzi
b) Mzazi/mlezi kukiri na kukubaliana na sharia kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
c) Medical Examination Form ambayo inajazwa na Mganga Mkuu wa serikali.
NB:Fomu hii inapatikana kwenye ukurasa namba 5(tano) fomu hii inakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

**5.0** Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB : KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJA NA MCHE MMOJA WA MTI WA MATUNDA, EMBE, KOKOMANGA, PARACHICHI, PERA N .K**

*KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MAILISITA*

..........................................................

JOSINA V. MISAGO
MKUU WA SHULE

HEADMISTRESS
MAILISITA SEC SCHOOL
P O Box 1734,MOSHI